



KONGAMANO LA TANO LA KISWAHILI LA KIMATAIFA

KIDOKEZO:

Baraza la Kiswahili la Zanzibar linatarajia kufanya Kongamano la Tano la Kiswahili la Kimataifa litakalowajumuisha pamoja wataalamu, wapenzi na wadau mbalimbali wa Lugha, Utamaduni na Fasihi ya Kiswahili kutoka maeneo mbalimbali duniani ili **Kutathmini Matumizi ya Kiswahili Kupitia TEHAMA kama Msingi wa Maendeleo Endelevu ya Kiswahili Kimataifa.**

SHABAHA YA KONGAMANO:

Kutathmini Matumizi ya Kiswahili kupitia TEHAMA kama Msingi wa Maendeleo Endelevu ya Kiswahili Kimataifa.

KAULI MBIU YA KONGAMANO:

Tumia TEHAMA katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Kimataifa.

MAKALA ELEKEZI:

Matumizi ya TEHAMA katika kufuatilia Fursa na Taaluma za Kiswahili.

SIKU YA KONGAMANO

JUMAMOSI - JUMAPILI

TAREHE

11 – 12 DISEMBA 2021

UKUMBI

SHEIKH IDRISA ABDUL-WAKIL

MAHALI

ZANZIBAR - TANZANIA

MADA KUU

TEHAMA KATIKA MAENDELEO YA KISWAHILI
DUNIANI.

MAWASILIANO

Simu: +255 777 873676

  @bakizanz

Tumia TEHAMA katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili

MADA NDOGONDOGO

1. Kiswahili/Fasihi na Teknolojia.
2. Kiswahili/Fasihi na Demokrasia.
3. Kiswahili/Fasihi na Uchumi
4. Kiswahili na Uchumi wa Buluu
5. Kiswahili/Fasihi na Mazingira.
6. Kiswahili/Fasihi na Vyombo vya Habari.
7. Kiswahili/Fasihi na Historia.
8. Kiswahili/Fasihi na Utalii.
9. Kiswahili/Fasihi na Jinsia.
10. Kiswahili/Fasihi na Sheria.
11. Kiswahili/Fasihi na Afya.
12. Kiswahili/Fasihi na Michezo.
13. Kiswahili/Fasihi na Vijana.
14. Kiswahili/Fasihi na Watu wenye Ulemavu
15. Kiswahili kwa Wageni na Teknolojia.
16. Makala kuhusu waandishi wa Fasihi na Isimu ya Kiswahili.

ITIFAKI YA UVIKO 19

Kutokana na hali isiyokuwa na uhakika iliyosababishwa na kuibuka kwa janga la Corona, Baraza litawataka washiriki wazingatie itifaki ya UVIKO 19 kikamilifu na kufuata maelekezo kama yatakavyotolewa na Serikali.

KATIKA KONGAMANO HILO WASHIRIKI WATAPATA FURSA YA KUFANYA UTALII WA KIFASIHI KATIKA ENEO LA MANGAPWANI

MAWASILIANO

Simu: +255 777 873676

  @bakizanz

UTUMAJI WA IKISIRI NA MAKALA

Ikisiri zote zitumwe kuanzia tarehe **30 Agosti 2021** hadi tarehe **30 Oktoba 2021**.

Ikisiri hizo ziwe na **maneno** kati ya **200** na **300** na **Makala** iwe na **kurasa** kati ya **kumi (10)** hadi **ishirini (20)** kwa hati ya 'Times New Roman' Ukubwa wa Hati **12** na Mwachano **1.5**.

Ikisiri na Makala zote zitumwe kupitia baruapepe kongamano2021@bakiza.go.tz

N.B:

Ikisiri na Makala zote zitumwe kwenye baruapepe iliyotajwa hapo juu na si vyenginevyo.

ADA YA KONGAMANO

Ada ya kila mshiriki kutoka nje na ndani ni Tsh. **60,000/-**

Ada hiyo itumwe kupitia akaunti ya benki

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

NAMBA YA AKAUNTI: 0406404000

JINA LA AKAUNTI: WVUSM

Tumia TEHAMA katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili